**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**BARAZA LA MADAKTARI TANGANYIKA**

# TAARIFA KWA UMMA
# KULAANI KITENDO CHA DAKTARI ALIYESABABISHA KIFO CHA MAMA MJAMZITO KATIKA KITUO CHA AFYA NGARENAIROBI WILAYANI SIHA, MKOA WA KILIMANJARO

Baraza la Madaktari Tanganyika limepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Mama mjamzito Bi. Dainess T. Massawe, kilichotokea tarehe 20/09/2023 katika Kituo cha Afya Ngarenairobi kilichopo Wilaya ya Siha, Mkoa wa Kilimanjaro.

Taarifa tajwa zinamtuhumu Daktari Msaidizi wa Kituo cha Afya Ngarenairobi, (Jina linahifadhiwa) kwamba alimhudumia marehemu akiwa kwenye hali ya ulevi na kwa kuchelewa hali iliyopelekea kifo cha mama huyo.

Baraza linatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu kwa kuondokewa na mpendwa wao. Aidha, Baraza linawasihi Wananchi Wilayani Siha kuwa watulivu na wavumilivu katika kipindi hiki ambacho kwa kushirikiana na Vyombo vingine linafanya uchunguzi wa kitaalam kubaini kilichopelekea kifo cha marehemu.

Baraza linaendelea kuwakumbusha wanataaluma ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi kutoa huduma stahiki na kwa wakati kwa wagonjwa kwa kufuata Sheria, Taratibu, na Kanuni za kitaaluma pamoja na kutumia taaluma zao kutibu watu.

**Roho ya marehemu Dainess T. Massawe ipumzike kwa amani.**

Dkt. David P. Mnzava
**MSAJILI – BARAZA LA MADAKTARI TANGANYIKA**
27/09/2023